BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba kuanza hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuendelea kukutana katika Baraza hili Tukufu ikiwa leo ni siku ya nne ya kikao hiki tukiwa tunatekeleza majukumu ya kulijenga taifa letu. Kwa hakika ni jambo la kujivunia kwani hii ni rehma yake Muumba kwa kutupa pumzi na uzima ambao wenzetu wengine amewanyima.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa ridhaa yako naomba nitoe shukurani kubwa kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kitendo cha kiungwana alichokionesha siku ya wafanyakazi Mei Mosi kwa kuongeza maslahi ya watumishi wa Serikali ya kuwapa nauli ya elfu hamsini kwa kila mwezi jambo ambalo litasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa changamoto ya nauli kwa ajili ya kuwahi kazini. Jambo hili linaonesha ukomavu wa kisiasa na uongozi na kwa namna bora anavyowajali wafanyakazi wa nchi hii. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amzidishie hekima, busara na upendo wa kuijali nchi na wananchi wote wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**,

Kwa moyo wa dhati kabisa, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kusimama mbele yako na kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu ***Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2024/2025***.

**Mheshimiwa Spika**,

Pia, natoa pongezi maalumu kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mheshimiwa Mwl. Haroun Ali Suleiman, ambaye kwa kiasi kikubwa anafanya kazi kwa kusaidiwa na Katibu Mkuu wake Ndg. Mansura Mosi Kassim, Afisa Mdhamini na watendaji wote kwa mashirikiano yao makubwa wanayoipatia Kamati hii, kuthamini maoni yao na kuyazingatia vyema katika utendaji wa Serikali. Nachukua nafasi hii kuwaomba waendelee na uzalendo wa kuisimamia wizara hii kwa maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kutumia fursa hii pia, kuwapongeza na kuwashukuru waheshimiwa Wajumbe wote waliomo katika Baraza lako Tukufu, kwa kuendelea kuwawakilisha na kuwatumikia wananchi waliowachagua. Ni wazi kwamba wananchi wamejenga imani kubwa kwetu, nasi hatuna budi kurejesha imani kwao kwa kuwatumikia kwa dhati na kwa moyo wetu
wote, bila ya kusahau kutetea maslahi yao katika Baraza hili na katika kipindi hichi cha upitishaji wa bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,**

Sasa naomba pia, kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu kwa michango yao mikubwa wanayoendelea kuipatia wizara na hasa katika kuyapitia mapendekezo ya bajeti ya Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2024/2025, kwa heshima ya kipekee naomba sasa kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Maryam Thani Juma | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Panya Ali Abdallah | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Haji Shaaban Waziri | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati hii inafanyakazi na makatibu watatu na Mkalimani wa Lunga za Alama ambao wamekuwa wakitusaidia kwa kiasi kikubwa na kwa uweledi wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yetu ambayo yametupatia mafanikio makubwa. Makatibu hao ni:-

| | | |
|---|---|---|
| 9. | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| 10. | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| 11. | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu |
| 12. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,**

Ni jukumu la msingi la kila kamati kuchambua mapendekezo ya Serikali, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara kwa kila mwaka, hivyo katika kutekeleza jukumu hilo lililoelezwa katika kanuni ya 97(1), Kamati yangu ilikaa na kuijadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, mnamo tarehe 02/05/2024 na leo hii, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati yangu, natumia fursa hii kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo kama ifuatavyo:-

**Mheshimiwa Spika,**

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 itatekeleza kazi zake kupitia mafungu ya bajeti 12 na Programu kuu 15. Maelezo ya kina kwa kila Fungu la Bajeti na Programu hizo ni kama ilivyowasilishwa katika Kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri hivi punde.

**Mheshimiwa Spika**,

Kwa upande wa **fungu G01** kupitia program kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Kamati inakipongeza Chuo cha Utumishi wa Umma (IPA) kwa jukumu la kuwaendeleza Watumishi wa Umma na Watumishi wa Sekta binafsi kupitia programu mbali mbali za chuo ambazo wanazoziandaa. Aidha, Kamati inakipongeza Chuo kwa hatua iliyofikia ya

maandalizi ya ujenzi wa tawi la chuo Pujini Kisiwani Pemba, kwani kukamilika kwa ujenzi wa chuo hicho kutasaidia kuondoa changamoto ndogo ndogo za uchache wa vyumba vya kusomea na ofisi kwa watumishi wa chuo. Kamati inaiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kutafuta mfadhili wa kuwapatia fedha kwa ajili ya kukamilisha jengo hilo kwa uharaka, na fedha hizo kurejeshwa kwa awamu mara jengo litakapomalizika.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji wa ahadi mbali mbali zinazotolewa kwa watumishi wa umma kwa lengo la kuboresha maslahi yao, kupitia Kifungu cha **PG0106** ***Programu kuu ya Usimamizi wa Rasilimali watu na Utumishi wa Umma*** kwa kufanya uhakiki wa mishahara kwa Mamlaka, Mashirika na Taasisi 22 zinazojitegemea zilizo chini ya Wizara nne (4), pamoja na kutambua kasoro zilizojitokeza katika ulipaji wa mishahara na posho na utekelezaji wa miundo ya utumishi ambazo zimerekebishwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Hata hivyo, kamati yangu inapata wasiwasi na kazi hii ambayo imefanyika kutokana na baadhi ya taasisi kuwepo kwa maombi na ushauri wa muda mrefu lakini hawajafanikiwa katika muktadha mzima wa maslahi. Hivyo basi, Kamati inashauri kuzingatia zaidi taasisi ambazo hadi sasa hazijatekelezewa maombi yao kwa kuzingatia mazingira magumu ya kazi na unyeti wa kazi husika. Aidha, Kamati inasisitiza marekebisho ya kimaslahi yanapofanyika kuzingatia uwiano baina ya taasisi na taasisi ili kuondoa kasoro zinazojitokeza kwa watendaji wa taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Imeelezwa kwamba kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Skuli ya Sheria imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi za kitanzania 1,012,500,000 kwa ajili ya ruzuku ya matumizi ya kawaida. Aidha, Skuli imepanga kukusanya Shilingi za kitanzania 179,500,000 kupitia malipo ya ada za wanafunzi na uendeshaji wa mafunzo mafupi. Kamati yangu inaisisitiza Wizara kuwa makini sana na utekelezaji wa matumizi ya fedha zitakazoingizwa kwa ajili ya taasisi hiyo, kwani licha ya uhaba wa fedha, matokeo ya fedha hizo yatahitaji kuonekana kwa vitendo.

Aidha, Kamati inaiomba Serikali kufanya utaratibu wa kuwapatia Skuli ya Sheria jengo la kudumu kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zake ili kuondokana na kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kulipa kodi ya ofisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka huu wa fedha ni Kuimarisha upatikanaji wa haki na utawala wa sheria, kusikiliza kesi na kutoa maamuzi ya haraka na kwa wakati. Kamati wakati ikiipitia bajeti ya **Fungu G02** la Mahakama Kuu kupitia programu kuu ya kifungu **PG0201** ilielezwa juu ya hatua nzuri iliyofikiwa katika ujenzi wa Mahkama za Mikoa na Wilaya kwa Zanzibar ambapo kamati imeridhika na maelezo iliyopatiwa.

Sambamba na hayo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuongeza idadi ya majaji na Mahakimu hususan kwa mahakama mpya zinazojengwa ambazo zitasaidia kupunguza mrundikano wa kesi za udhalilishaji na dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati inaipongeza Mahakama Kuu kwa kuandaa Muongozo wa Jaji Mkuu wa mwaka 2024 ambao utasaidia kuwaongoza waheshimiwa Majaji na Mahakimu

kusimamia uendeshaji wa kesi, kwa kuangalia namna muda gani mashauri hayo yanapokelewa yanaendeshwa kwa wakati pamoja na hatua za kinidhamu kwa hakimu ataecheleweshа mashauri hayo.

Kwa upande mwengine, Kamati inashauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mahakama Kuu kutafuta njia muafaka itakayoondosha changamoto ya utambulisho wa cheti cha Uwakili kwa upande wa Mawakili Mahakama Kuu Tanzania Bara ili kutambulika Zanzibar, na cheti kinachotolewa na Skuli ya Sheria Zanzibar kutambulika rasmi Tanzania Bara kwani wote hawa wanafanya kazi kwa ajili ya kusimamia haki na kuleta maendeleo ya utawala wa kisheria katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika **fungu G03** Afisi ya Mwanasheria Mkuu linatekeleza kazi zake kupitia ***Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa huduma za Sheria.*** Kamati inaipongeza Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa Kuendelea vyema kusimamia na kutekeleza Mikataba ya Serikali kikanda na kimataifa pamoja na kutoa ushauri wa kisheria katika Hati za Maelewano (MoU); Kamati ilipata nafasi ya kutembelea taasisi mbali mbali na kusikia changamoto zinazowakabili kwenye suala zima la Mikataba ambayo hupelekwa katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kuihakiki na kupata ithibati ya Mwanasheria Mkuu.

Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa baadhi ya taasisi wanacheleweshа kupeleka mikataba yao katika Afisi ya Mwanasheria kwa ajili ya kutimiza matakwa ya kisheria. Kwa maana hiyo, kamati inashauri watendeji wanaohusika na utayarishaji wa mikataba katika taasisi za Serikali kupata elimu ya ushauri juu ya muda sahihi wa kutuma mikataba yao kwenye afisi hii na namna bora ya uandishi ili mikataba hiyo imalizike kwa muda sahihi na bila ya hasara yoyote kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, kupitia Programu zake imepangiwa kutumia Shilingi **5,445,600,000** bilioni kwa ajili ya mishahara na matumizi ya kawaida. Aidha ruzuku ya Shilingi Milioni **190,400,000** imepangwa kutumika kwa ajili ya Kituo cha Utafiti wa Sheria. Kamati inaiomba Serikali kupitia Bajeti hii kufungua Afisi za Mikoa ili kutekeleza kwa urahisi jukumu la Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai kwa Unguja na Pemba. Aidha, Kamati inasisitiza kuendelea na vikao vya taasisi za haki jinai ili waweze kutatua changamoto za kesi zinazojitokeza katika taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana yenye **Fungu G12** katika program zake inazotekeleza ina jukumu la kusimamia na kuendesha Mali za Wakfu na Amana, kuendesha mirathi ya marehemu wa kiislamu, kuratibu shughuli za Hijja, ugawaji wa sadaka, Zakka na misaada ya kheri.
Kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 fungu hili limepangiwa kufanya mapitio ya Sheria ya Wakfu na Muundo wa Taasisi, kuendeleza Miradi na Uwekezaji wenye Tija. Kamati inaipongeza Kamisheni kwa kusomesha watendaji sita wa mafunzo ya uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Kamisheni katika nchi za Oman na Malaysia ili waje kuisaidia taasisi hii katika misingi ya Dini ya Kiislam. Aidha, Kamati inaiomba Serikali kuyafanyia haraka marekebisho ya Sheria yao ili kuondosha mapungufu yanayojitokeza katika utekelezaji wa kazi zao hususan katika masuala ya kiuchumi na kijamii.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini, Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar kwa mwaka 2024/2025 imepanga kuimarisha uratibu na usimamizi wa

mambo ya kiislamu na kuzijengea uwezo taasisi za kiislamu, kuimarisha shughuli za kiislamu na kinga juu ya haki za wanawake na watoto. Aidha, Kamati wakati ikitekeleza kazi zake za ufatiliaji wa bajeti kwa mwaka 2023/2024 ilipata fursa ya kutembelea Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar ikiwemo ukarabati wa jengo la ofisi yao pamoja na kupata elimu wa masuala kadhaa juu ya usimamizi wa masuala ya Dini. Sambamba na hilo, kamati ilitembelea Msikiti na Madrasa ambayo hutumika kwa ajili ya kutoa elimu kwa wanandoa na kutoa elimu ya msingi kwa watu wanaosilimu.

Viulevile, kamati imeridhika sana na hali ya utulivu wa kidini uliopo Zanzibar kwa sasa. Hivyo basi, kamati inatoa shukurani na pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Mufti Mkuu wa Zanzibar pamoja na Katibu Mtendaji wa Ofisi hiyo Sheikh Khalid Ali Mfaume. Kiujumla kamati inawatakia kila la kheri katika kusimamia taasisi hii muhimu pamoja na kuwaombea kwa Serikali kuwaingiza fedha zao kwa wakati ili waweze kukamilisha malengo yao waliyojiwekea .

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa **fungu E05:** katika ***Programu Kuu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi,*** Kamati inaipongeza Mamlaka kwa utekelezaji mzuri wa kazi zao za udhibiti wa vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi ili kuhakikisha fedha za Serikali zinatumika kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa.

Kwa mantiki hiyo, kamati inaiomba Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kupatiwa fedha za kutosha na kwa wakati ili kutatua changamoto ambazo zinawakwaza katika uendeshaji wa shughuli zao za kila Wilaya kwa lengo la kuleta ufanisi. Aidha, kamati inaitaka Mamlaka hii kufanya kazi kwa weledi, hekma na busara katika kufuatilia kesi za uhujumu uchumi kwa taasisi za umma na kuhakikisha kwamba haki ya kila mtendaji inalindwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

HITIMISHO:

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya maoni hayo ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, ambayo yamejikita katika programu kuu na ndogo, na baada ya hotuba nzuri iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri, ni tumaini langu kuwa wizara hii itatekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Pamoja na maoni haya machache, tunawaomba wajumbe wengine wa Baraza lako tukufu, waichangie vyema bajeti hii, kwa lengo la kupata utekelezaji bora wenye maslahi kwa wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho kabisa, napenda kukushukuru tena, wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati, pamoja na kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa, sasa niwaombe Wajumbe wa Baraza hili waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii, ili wamuwezeshe Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliyojipangia katika mwaka
huu wa Fedha wa 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** kwaniaba ya Kamati yangu ya kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, **Naunga Mkono Hoja , na naomba Kuwasilisha**

**Ahsante,**

……………………………………

(Machano Othman Said)

MWENYEKITI,

KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA,

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR